

HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

MKOA WA MARA

Simu Na. + 255 (028) 2621264
Nakushi Na:+225(028)2621055
Email:td.bunda@mara.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji,
Halmashauri ya Mji wa Bunda,
S.L.P 219.
BUNDA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.HMB/H:10/12/26

23 Machi, 2018

Wananchi Wote

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Bunda anapenda kuwatangazia Watanzania wenye sifa za kuomba nafasi za kazi ya Watendaji wa Vijiji kwa Masharti ya Kudumu. Tangazo hili ni baada ya kupokea **kibali cha ajira mbadala chenye Kumb.Na.CFC 26/205/01 "F"/91 cha tarehe 22/8/2017** pamoja na barua ya nyongeza ya muda wa utekelezaji wa kibali cha ajira mbadala kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa chenye **Kumb.Na.CFC.26/205/01 "GG"/95 cha tarehe 12/03/2018** vyote kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mchanganuo wa nafasi ni kama ifuatavyo:-

i.Afisa Mtendaji wa Kijiji Daraja III – (Nafasi – 13).

- Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne au Sita.
- Awe amepata mafunzo ya stadi za kazi katika ngazi ya Cheti (NTA Level 5) ambao wamehitimu katika maeneo yafuatayo:-

Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo Kingine Chochote kinachotambulika na Serikali.

ii.Mshahara.

- Atakayeajiriwa na Elimu ya Ngazi ya Cheti ataanza na Mshahara wa TGS B1. sawa na Tshs.390,000.00 kwa mujibu wa Waraka wa Mshahara serikalini wa mwaka 2015/2016.

iii. Majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kijiji III.

- a) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- b) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- c) Kuratibu na kusimamia upangaji wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Jamii.
- d) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- e) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- f) Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamamisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- g) Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika Kijiji.
- h) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- i) Kuwa Mwenyekiti wa kikao cha Wataalam waliopo katika Kijiji.
- j) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi.
- k) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji na
- l) Utawajibika kwa Mtendaji wa kata.


MASHARTI YA JUMLA YA MUOMBAJI KAZI.

- Awe Raia wa Tanzania
- Awe na miaka 18 – 45.
- Awe hajawahi kufukuzwa kazi, kupunguzwa, kuachishwa au kustaafishwa kazi katika Utumishi wa Umma.
- Awe tayari kufanya kazi Kijiji chochote ndani ya Halmashauri ya Mji wa Bunda.
- Waombaji waambatanishe vivuli vya vyeti vya Shule, Taaluma, Cheti cha Kuzaliwa na vitambulisho vya Taifa kwa wale waliondikishwa.
- Curriculum Vitae (CV) – Taarifa binafsi ya mwombaji
- Mwombaji mwenye cheti cha kughushi asijaribu kuomba nafasi hizi, endapo atabainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
- Kila mwombaji aambatishe picha ndogo 2 (Passport Size) zilizopigwa hivi karibuni.
- Siku ya usaili kila mwombaji afike na vyeti halisi vya Shule, Taaluma, kuzaliwa na Kitambulisho.
- Kila Mwombaji aandike kwa usahihi anwani yake na namba yake ya simu inayopatikana kwa muda wote kwa ajili ya mawasiliano.
- Mwisho wa Kupokea maombi ni tarehe 05/04/2018.
- Maombi yote yaandikwe kwa Mkono bila kuchapwa.

- Maombi yote yawasilishwe kwa anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji,
S.L.P 219,
BUNDA

NB: Masharti yaliyoainishwa kwenye Tangazo hili yasomwe kwa makini na yazingatiwe.


Janeth P. Mayanja
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
BUNDA



Nakala: Katibu Tawala (M),
MKOA MARA

-“- Waheshimiwa Madiwani,
Halmashauri ya Mji,
BUNDA

-“- Watendaji wa Kata Wote,
Halmashauri ya Mji,
BUNDA

-“- Soma Website ya Halmashauri ya Mji,

-“- Mbao za Matangazo Zote
HALMASHAURI YA MJI BUNDA